

NDOTO YAKO INAWEZEKANA

TIMOTH J. KYARA

TIMOTH KYARA
NDOTO YAKO INAWEZEKANA



www.hekimatalk.co.tz

©Timoth J Kyara, August 2020

MENENO ya UTANGULIZI kutoka kwa:

Dr. Deo Lubala

Dr. Chris Mauki

Mrs. Luphurise Mawere

Mr. Mosses Raymond


NDOTO YAKO INAWEZEKANA

Kitabu hiki kimeandikwa na,

Timoth Japhethy Kyara
P. O. Box 2524, Ilala,
Dar Es Salaam, Tanzania
www.hekimatalk.co.tz

Toleo la Kwanza, August, 2020

Haki zote zimehifadhiwa



Cover Design By:

Aidan Magomba
Maestro – Graphics and Branding Agency

Printed By:

Niim Printers & Media Services

Published By:

©Timoth J. Kyara, 2020

ISBN

978-9987-780-10-5

Online Resources from Hekima Talk | Tim Kyara:

www.hekimatalk.com

www.timkyara.blogspot.com

www.light2mypath.blogspot.com

www.timkyara.wordpress.com

www.laughin2health.blogspot.com



MWAKA 2019 COCACOLA WALITUMIA USD 4BN (TSH 9TRILION) KWENYE MATANGAZO YAO YA BIASHARA. WANACHO KITAFUTA, KAMA MAKAMPUNI MENGINE, NI KUKAMATA **AKILI** NA **HISIA** ZAKO ILI WAENDELEE KUKAMATA SOKO LA VINYWAJI. ILI UWEZE KUTIMIZA NDOTO YAKO, ITAKUPASA KUTUMIA AKILI NA HISIA ZAKO VIZURI.



Mpendwa Msomaji...

Nakushukuru sana kwa kuchukua uamuzi muhimu wa kusoma kitabu hiki!

Nafasi haiwezi kutosha kumshukuru kila mtu mmoja mmoja aliyenisaidia na kunishika mkono mpaka hapa nilipofika leo. Kitabu hiki kisingeweza kutoka kama asingekuwa ushirikiano wa dhati na changamoto kutoka kwa mke wangu **Irene Robert Ungani** na watoto wetu **Axel** na **Amaris**.

Pia nawashukuru wazazi wangu, **Askofu Japheth Kyara** na **Ruth Gladness Kyara**, kunilea vyema na kunifanya kuwa tunu kwa kila mtu ninaye kutana naye.

Mbegu njema waliopanda maishani mwangu kwa maneno, matendo na mahali walipotulea mimi na ndugu zangu (**Grace Japheth-Mfinanga**, **Joshua Kyara**, **Fred Kyara**, **Daniel Kyara**, **Gideon Kyara** na **Aaron Kyara**), imekuwa chachu ya kuniweka kwenye nafasi niliyopo leo.

Asante sana Mama na Baba, Ruth na Japheth Marko Kyara.



AFIKIRIAYYO (AJIONAVYO NA KUJIDHANIA)
MTU NAFSINI | MOYONI MWAKE, NDIVYO
ALIVYO MAISHANI

BIBILIA, MITHALI 7:23B, TAFSIRI NA MSISITIZO WANGU



Maalum Kwenu Wanafunzi Wangu!

Kitabu hiki ni maalum kwa wanafunzi wangu wote ***Dreamers Summit, Hekima Talk*** na ***Hekima Mastermind Groups***. Nimekitoa kitabu hiki maalum kwenu (na watoto mtakao wazaa) kama sehemu yangu ya kuendelea kuwa mwalimu na msaidizi wenu mpaka ndoto na kusudi lililowekwa ndani yenu litimie.

Nawapenda na nimetamani kuona kazi yenu ikizaa matunda na kufanikiwa sana kuliko niwezavyo kuwaza au kutenda – kama Mungu aishivyo na kutujalia.

Ni Mimi,

Mwalimu Wenu,

_Tim Kyara
August, 2020



YALIYOMO

1:: UTANGULIZI – MSINGI MUHIMU	12
1.1 Ndoto ni Nini?.....	18
1.2 Namna ya Kuamini Ndoto Yako.....	27
1.3 Kutimiza Ndoto ni Safari ya Maisha.....	35
2:: WEWE na NDOTO YAKO	46
2.1 Umuhimu wa Kujitambua Nafsi Yako	48
2.2 Umuhimu wa Kutambua Ndoto Yako.....	49
2.2.1 Kuondoa Upofu Ndani Yako	50
2.2.2 Kujiandaa Mapema kwa Yajayo	52
2.2.3. Kuondoa Hofu ya Mambo Yajayo.....	54
2.3 Umuhimu wa Kutambua Kusudi la Ndoto Yako.....	56
2.3.1 Utayari kulipa Gharama Ufanikiwe	56
2.3.2 Uvumilivu na Subira unapopitia Magumu,	58
2.3.3 Unyenyekevu na Usikivu utakapo Fanikiwa	60
2.4 Jitambue na Jikubali Nafsi Yako.....	62
2.4.1 ROHO – Uhai, Ufahamu, Umilele	71
2.4.2 NAFSI – Akili, Hisia na Utashi	72
2.4.3 MWILI – Milango Mitano ya Fahamu, Uzima na Afya	83
2.5 Itambue na Ikubali Ndoto Yako	88
2.5.1 Namna ya Kutambua Ndoto Yako.....	88
2.5.2 Ijaribu na Kuithibitisha Ndoto Yako	94
2.5.3 Namna ya Kuikubali Ndoto Yako	103

2.6 Tambua na Tumikia Kusudi la Ndoto Yako	109
3:: AMKA UTIMIZE NDOTO YAKO	121
3.1 Ndoto Yako Inawezekana	125
3.2 Namna ya Kutimiza Ndoto Yako.....	128
3.2.1 <i>Ingiza Ndoto Yako Ndani</i>	138
3.2.2 <i>Fuata Maelekezo Yako Maramoja</i>	150
3.2.3 <i>Weka Nidhamu ya kuwa na Kipaumbele</i>	153
3.3 Mambo Sita ya Kufahamu Utimize Ndoto Yako	155
3.3.1 <i>Wazo lako lazima liwe Bayana kwako</i>	155
3.3.2 <i>Unahitaji Msukumo (Shauku) yako iwe Mkubwa</i>	156
3.3.3 <i>Unahitaji Mshauri na Kocha Wako</i>	157
3.3.4 <i>Unahitaji kuwa na Nidhamu na Msimamo</i>	159
3.3.5 <i>Unahitaji Matendo kufuata Ndoto Yako</i>	161
3.3.5 <i>Unahitaji kuweka Fedha na Muda wa Ndoto Yako</i>	163
3.4 Lipia Gharama Utimize Ndoto Yako	164
3.5 Ndoto Yangu kuwa Mwalimu wa Wengi	169
4:: WEKA MIKAKATI UTIMIZE NDOTO YAKO	180
4.1 Jitambue na Ujikubali – 100%.....	181
4.2 Tambua na Kubali Ndoto Yako – 100%	185
4.3 Andika Ndoto Yako Uione kila Siku	186
4.4 Tamka, Jiongeleshe Ndoto Yako Kila Siku	189
4.5 Fanyia Kazi Maelekezo Unayopata Kila Siku	191
4.6 Kaa na Watu mnaofanana Mitazamo	193
4.7 Tenga Akiba ya Fedha ya Ndoto Yako	196
4.8 Ndoto yako ni Haki Yako , Usikate Tamaa	199

5:: FANYIA KAZI MIKAKATI YAKO	208
5.1 Tenga Muda wa Tafakari Kila Siku	209
5.2 Tembea na Uaminifu, Uvumilivu na Subira	211
5.3 Semina za Motisha na Misukumo	213
5.4 Jenga Nidhamu ya Kazi	217
5.5 Fanyia Kazi Kanuni ya 80 20.....	219
5.6 Mbegu kutoka Mbinguni	221
6:: JIFUNZE KWA WALIOTANGULIA.....	229
6.1 Jifunze Toka kwa Watu Hawa	230
6.1.1 <i>Wazazi au Walezi Wako</i>	231
6.1.2 <i>Ndugu wa Karibu na Marafiki</i>	236
6.1.3 <i>Viongozi wako wako wa Kazini, Dini au Kiasasa</i>	239
6.1.4 <i>Vitabu vya Maisha ya Waliofanikiwa</i>	240
6.2 Tabia Kumi za Watimiza Ndoto	242
7:: MAMBO 8 YANAYO ZUIA NDOTO YAKO	254
7.1 Kuto Kufahamu na Kuikubali Ndoto Yako	256
7.1.1 <i>Malengo Yasiyo Bayana</i>	257
7.1.2 <i>Msukumo Hafifu toka Ndani</i>	258
7.1.3 <i>Wauwaji wa Ndoto Yako</i>	259
7.1.4 <i>Historia ya Kushindwa</i>	260
7.1.5 <i>Kutamani Maisha ya Wengine</i>	260
7.2 Nafsi na Akili Isiyofundishika	263
7.3 Sababu Hafifu Msukumo Dhaifu wa Ndoto	264
7.3.1 <i>Majukumu ya Mpito - Yachangamkie</i>	265
7.3.2 <i>Mwelekeo ambao sio wako - Badilika</i>	265


7.3.3 Kutoelewa au Kutokubali Kulipa Ndoto Yako	266
7.4 Magonjwa 5 Hatarishi ya kwenye Nafsi ya Mtu	267
7.4.1 Mashaka na Kutojiamini.....	268
7.4.2 Kusita-sita, kuwa na Kauli Mbili	269
7.4.3 Mtazamo Hasi Muda Wote	271
7.4.4 Kulalamika na Kunung'unika	272
7.4.5 Tahadhari ya Kupita Kiasi	275
7.5 Kutoendeleza Kipaji na Kutotumia Fursa Vizuri	278
7.6 Marafiki Wasiofaa kwa Mwelekeo Wako	279
7.7 Falsafa Potofu za Mafanikio ya Maisha	281
7.8 Hofu ya Kutoka Nje ya Mazoea	287
8:: VITABU VYA KUSOMA UJIFUNZE ZAIDI.....	296
8.1 Kwa nini Nisome Vitabu	299
8.2 Vitabu vya Kuanzia Navyo	302
9:: HITIMISHO.....	315
9.1 Fanya Maamuzi Yako Mwenyewe	316
9.2 Shukurani.....	319



UKIAMINI, YOTE YANAWEZEKANA
KWAKE YEYE AAMINIYE

YESU KRISTO, MARKO 9:23, TAFSIRI NA MSITIZO WANGU





JAMBO LOLOTE UNALO LITAMANI (FIKIRIA,
WAZA, LIOTA) UKIWA UNAONGEA NA
MUNGU (MAOMBI), AMINI UNALO, WAKATI
HUO UNAPO OMBA, NA LITAKUWA LA KWAKO

YESU KRISTO, MARKO 11:24, TAFSIRI NA MSISITIZO WANGU





*Moja wapo ya **NJIA** ya Kujifunza kitu kipya ni **KURUDIA** tena na tena **KUSOMA** kitu kile kile. Nakualika usome kitabu hiki – tena na tena – mpaka mafunzo yaliyomo humu ndani yaingie ndani ya nafsi yako.*

*Ni kwa sababu hii, **nimerudia rudia** baadhi ya mambo ninayofundisha humu, si kwa bahati mbaya bali ni kwa makusudi kabisa kama njia mojawapo ya kukusaidia **kuelewa** na **kukumbuka** somo ili **uyafanyie kazi** ufanikiwe.*





IMANI NI UHAKIKA WA MAMBO
YATARAJIWAYO (YAKUFIKIRIKA, MAWAZO,
NDOTO) NI UHAKIKA WA KUWA NA MAMBO
AMBAYO HAYAJAONENAKA KWA MACHO YA
MWILI.

BIBILIA, WAEBRANIA 11:1, TAFSIRI NA MSISITIZO WANGU



Ndoto Yangu Juu ya Kitabu Hiki


*Moja ya ndoto yangu kubwa ni kuweka hiki kitabu mikononi mwa **watu milioni moja**, ambao baada ya kujifunza hili somo watawafundisha na wengine, kila mtu angalau watu wawili na hao wawili wataenda kuwafundisha wengine wawili . . . na kuendelea hadi kufikia zaidi ya **watu milioni mia moja** ndani ya miaka mitano kuanzia sasa!*

_Tim Kyara
August, 2020



AJIFIKIRIAYYO MTU NAFSINI MWAKE
(USHAWISHI, IMANI YAKE) KUHUSU YEYE,
NDIVYO ALIVYO (MATENDO NA MATOKEO)

MFALME SULEMANI, MITHALI 23:7, TAFSIRI NA MSISITIZO WANGU



Ndoto Yangu Juu yako Msomaji

*Ndoto yangu na shauku yangu ni kuwa **UTASOMA KWA MAKINI** na **KUJIBU MASWALI YOTE 50** yaliyowekwa ndani ya kitabu hiki kwa ustadi mkubwa kila mwisho wa sura. Kuwa utasoma kitabu hiki zaidi ya mara mbili na utajifunza mengi na mwisho wa siku utaweza kutimiza ndoto zako zote.*

*Ndoto yangu ni kuwa **KILA atakayesoma kitabu hiki na KUFANYIA kazi, MAISHA yake**, na ya wale walio karibu naye, **YATABADILIKA** kabisa kama usiku na mchana. Sio kwa sababu ya kitabu tu, lakini kwa sababu ya **KANUNI** ambazo kitabu hiki kinatukumbusha.*

***_Tim Kyara**
August, 2020*



*“Hatuchagui ndoto zetu,
tunachagua fikra
|mawazo|; fikra
zilizochaguliwa huvuta
ndoto linganifu kwetu na
maisha ya fikra zetu”
_Tim Kyara*

Kwa takwimu zetu Tanzania (2017), Mtanzania anategemewa kwa wastani kuishi miaka 65. Tukichukulia kuwa huu ndio umri watu wetu wengi wataishi, inabidi kila mtu ajipange katika muda huo.

Ukipata nyongeza, unamshukuru Mungu. Hivyo basi, miaka 10 ya mwanzo kwa sehemu kubwa maamuzi|fikra hufanywa na mzazi au mlezi, miaka 15 inayofuata kwa sehemu kubwa tunakuwa tupo ama shuleni/chuoni au tumeanza kazi/biashara ambayo inaamua Maisha yetu yaendeje.



Kwa mantiki hiyo, ukiondoa miaka 25 ya awali na miaka 10 ya mwisho; tunabakiwa na miaka 30 tu kwa ajili ya ***kufanya kitu ambacho nafsi inapenda***. Miaka 30 ni sawa na kusema unaishi sikukuu ya Pasaka au Iddi 30 tu baada ya hapo unaelekea kwa wahenga kupumzika.

Kwa maana nyingine, ni vema ukafikiria vile unavyo tumia muda, akili na rasilimali ambazo ziko kwenye mamlaka yako.

Nimesema haya ili kukumbusha hatuna muda mwingi hapa duniani, kufumba na kufumbua unaitwa **babu|bibi** – *unatembea na jimbo* – na mara tu unapumzika na wahenga.

Hivyo basi, **TUMIA MUDA WAKO VIZURI**, na ikiwa una jambo unapenda kulifanya, na katika kulifanya kwako hutadhulumu mtu haki yake, hakikisha **UNALIFANYA SASA HIVI** usingoje ruhusa kutoka kwa mtu yeyote.

Wengi wetu tunaishi Maisha yasiyo ya kwetu kwa vile tunaogopa,

*i. Hatuta-**eleweka**,*

*ii. Hatuta-**kubalika**,*

*iii. Hatuta-**thaminiwa** n.k.*

HOFU imekushika na kukukaba mpaka unaishi kama mgeni kwenye nyumba yako mwenyewe. **AMKA LEO UISHI MAISHA YAKO**, uvae nguo zako, ufanye furaha zako, ufanye kusudi lako, uwe na rafiki zako...muda si mrefu utaondoka!

Nikuambie kitu mtu wangu, “**Ndoto yako, Inawezekana**” Mtu akikuuliza, mwambie **USINISUMBUE TENA**, “*My Life, My Dream*” haya ni “*Maisha Yangu, Ndoto Yangu*” kataa kuishi kwa hofu kama watu wengine wengi, “*Hofu imeshika wengi wasithubutu kufanya kile wanachojua wanapaswa kufanya*”

Tim Kyara aka Mwalimu Kyara



MSHINDI NI MTU MWENYE NDOTO
ASIYEKATA TAMAA

NELSON MANDELA





SURA YA KWANZA. I

“Maisha hubeba maajabu ya kipekee kwa watu wenye uthubutu na ndoto zao”_Mithali

1:: UTANGULIZI – MSINGI MUHIMU

“Maisha hubeba maajabu ya kipekee kwa watu wenye uthubutu na ndoto zao”_Mithali za Wahenga Ulaya

Kizuizi namba moja cha watu wengi kutimiza ndoto zao ni *‘kutokuwa na imani’*, na hapa siongelei Imani ya kimungu au mambo ya rohani; naongelea kukosa Imani (*ushawishi wa ndani ya nafsi ya mtu*) kuwa anaweza **kuwaza, kutamani** na **kufanyia** kazi **wazo lake** likatimia. Watu wengi hatuna Imani kuwa ndoto zetu zinaweza kuwa halisia,

hivyo **hatujisumbui** kuzifuatilia maana **tunafikiri** ni kupoteza muda; bora tuendelee na **LOLOTE LILE** lililopo mbele yetu.

Ukweli ni kwamba, hatukuzaliwa hivyo; *uliza mtoto mdogo yoyote* ambaye bado fikra zake hazija haribiwa na *watu* au *mazingira*; utaona jinsi uso wake unavyong'aa na **matumaini** na **shauku** kuwa siku moja akiwa mkubwa atafanya hiki na kile.

Utakuta mtoto mdogo kutoka familia ya kimasikini kabisa akiwaza kuwa, *'nikiwa mkubwa nitajenga hospitali na kusaidia mamilioni ya wagonjwa bure au kwa gharama nafuu'*.

Kwa mtoto mdogo, mipaka na mapungufu ya kabila lake, umri wake, elimu yake, ukoo aliotoka, rangi yake au hata dini na dhehebu lake, havioni vyote hivi kama vina uzito katika kutimiza ndoto yake.

Ndani ya nafsi yake anafahamu kuwa kitu chochote anachotamani kufanya, akaamua kukifanya, kitafanikiwa – mwisho wa Habari. Na pia anafahamu, hata akikwama, wazazi, ndugu au marafiki zake wapo, watamsaidia mpaka atimize shauku yake.

Shida inaanza pale anapofikia umri wa **kuelewa mambo anayoyaona**; hapo ndipo anaanza kupata maarifa (mapya),

kulingana na uelewa wa **wazazi au walezi** wake na **mazingira aliyopo**, kuwa jambo alilokuwa anatamani haliwezekani – pia atapewa sababu za msingi, kwa mtazamo wao, kwa nini jambo analotamani kufanya haliwezekani.

Wakati huu ndio anakutana na watu wazima, wenye uzoefu (*waliokula chumvi nyingi*) wanaanza **kumpa masomo na kumkaripia** wakisema, '**acha utoto**' au '**acha ujinga**', '*hayo mambo unayowaza hayawezeke kiuhalisia – kwa mtu kama wewe.*' Kwa maneno ya tofauti tofauti, wanaivunja na kuiua ile ndoto ndani ya mtoto huyu.

Wanaweza wasiseme kwa mdomo, lakini matendo yao na sura zao zinatoshia kabisa kupeleka ujumbe kuwa ndoto zako ni za mwenda wazimu – **achana nazo**. Na kwa vile wamekutangulia, wamekuzaa au kukulea, ni kawaida kabisa kuamini kuwa wanachosema ni sawa – hivyo unaachia ulichokuja nacho na kupokea ulicho kikuta kwao; bila kujua hata wao walipokea kwa waliotangulia baada ya kuachia vya kwao.

LEO naomba **unipe ruhusa** nikurudishe utotoni, fikiria ndoto ile ulikuwa nayo wakati ukiwa mtoto; halafu **niruhusu NAFSINI kwako nikuambie UKWELI kuwa – NDOTO YAKO INAWEZEKANA**. Kumbuka, hapa sizungumzi kidini wala kiroho,

naongea kawaida kabisa kuwa – **JAMBO lolote unalo liwaza, ukiamini na kulifanyia kazi, linawezekana.**

Kumbuka wahenga walisema wazi kabisa kuwa mahali popote “Penye **NIA**, pana **NJIA**”. Huu ndio ukweli usiopingika unaosemwa kwenye mila na desturi za Waafrika, Waarabu Na Wazungu pia. Unapokuwa na nia ya kitu fulani, njia hupatikana; kama nia haipo au ni hafifu, njia huwa ngumu kupatikana.

Kwa hiyo shida ipo kwenye **NIA** ya mtu, na nia inakaa kwenye **NAFSI**; kama nafsi haijapata **NURU** ya jambo fulani, yaani **UFAHAMU**, haiwezi kuachilia **NIA** ifanye kazi yake ya kulitimiza. Somo lililopo kwenye kitabu hiki litakusaidia ili uweke **NURU** kwenye **NAFSI** yako ili upate kuachilia **NIA** ili uweze kufanya kazi yake ya kutimiza **NDOTO** zako, haijalishi kama ni kubwa au ndogo kiasi gani.

Nia ikiwa **HURU**, lazima ipewe **MWELEKEO**, huo mwelekeo ndio tunaita **NDOTO**; baadae tutaona kuwa ndoto ni **fikra**, **mawazo** au **malengo** uliyonayo na unayopenda au **unayosukumwa** kuyatimiza kwa manufaa yako na wengine. Ufahamu kabisa, hizi fikra, mawazo na malengo, havijaletwa kwako kwa bahati mbaya!!!

NDOTO YAKO INAWEZEKANA – TIM KYARA

Kumbe kiwango cha **NURU**, yaani **UFAHAMU**, nilicho-nacho ndani ya **NAFSI** (*FIKRA au nyumba ya MAWAZO yangu*) kitaamua uwezo wa kufikiri na hatimaye kufanya **MAAMUZI** na matokeo ya Maisha yangu.

Matokeo mabaya (au hafifu) hutokana na maamuzi mabaya, maamuzi mabaya hutokana na fikra (mawazo) mabaya, na mawazo mabaya au hafifu hutokana na ufahamu pungufu – **KIWANGO** na **UBORA** wa **NURU** (ufahamu).



Ndio maana ni muhimu sana kuongeza **KIWANGO** na **UBORA** wa **NURU** (**UFAHAMU** | **UJUZI**) ulio nao kuhusu jambo unalotaka kutimiza. Ukitaka kuwa fundi bora wa magari, lazima uongeze ufahamu (*kiwango na ubora*) wako kuhusu hilo eneo; ukitaka kuwa kiongozi bora, lazima uongeze kiwango na ubora wa ufahamu ulio nao kuhusu uongozi.

Dr Miles Munroe (1954-2014), Mwandishi wa vitabu, Mhubiri na Kiongozi Mshauri, aliwahi kusema kwenye mafundisho yake, *“Huwezi kuinuka juu ya kiwango cha uwezo wako wa*

kufikiri na kupambanua mambo. Kubadili maisha yako, lazima ubadili akili, mawazo na fikra zako”.

Dr Munroe anasema, huwezi kufanya jambo lolote juu (au nje) ya **kiwango chako cha kufikiri** – kubadili maisha yako lazima ubadili akili yako na mawazo (fikra) yako. Ili ubadili akili|fikra|mawazo yako, inabidi ubadili taarifa unazopokea.

Albert Einstein (1879-1955), Mwanasayansi Mjerumani mwenye asili ya Kiyahudi, alisema, “*Hatuwezi kutatua matatizo yetu kwa kiwango kile kile cha fikra | akili | mawazo tulivyokuwa nacho wakati tunayatengeneza”*

Kumbe basi, 1. *Matatizo tuliyonayo tumeyatengeneza kulingana na kiwango na ubora (uhafifu) wa fikra zetu,* 2. *Kuyatatua haya matatizo, lazima tubadili kiwango na ubora wa fikra zetu tulizonazo,* 3. *Ukiendelea kujaribu kutatua matatizo yako, kwa fikra ile ile iliyo yatengeneza, utatengeneza matatizo juu ya matatizo.*

Dr Martin Luther King Jnr. (1929 – 1968) alisema, “*I have a dream*”, kiswahili chake, “*Nina Ndoto*” au nina wazo, fikra na picha kichwani mwangu kuhusu maisha ya mbeleni ya mtu mweusi Amerika. Dr King Jnr, hakuwaza tu, alisema, akatangaza